## 1.0 UTANGULIZI

Bandari Kavu  ni eneo maalum (lisilo na bahari wala ziwa) linalotumika kwa shughuli zote za bandari kama vile kupokea na kutoa mizigo inayoingi na kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi, chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

### 1.1 Shuguli zinazofanywa Bandari kavu

Katika bandari kavu shughuli zifuatazo zinafanyika ili kuhakikisha kuwa mizigo yote inayotoka na kuingia nchini haipotei  na kulipiwa ushuru (kodi) kulingana na thamani ya mzigo husika:

- Kupokea na kuhakiki idadi ya mizigo inayoingia
- Kufanya ukaguzi wa mizigo yote inayoingia na kutoka nchini
- Kuimarisha ulinzi wa mizigo yote inayoingia na kutoka nchini
- Kutunza kumbukumbu  na taarifa ya kila mzigo unaoingia na kutoka nchini
- Kutoza ushuru (kodi) kwa kila mzigo unaoingia na kutoka nchini

## 2.0 UJENZI WA BANDARI KAVU NYANDA YA JUU KUSINI

Nyanda ya Juu Kusini mwa Tanzania inajumlisha mikoa saba (7) ambayo ni; Mkoa wa Mbeya, Songwe, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Iringa na Njombe. Kiuchumi eneo la nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa taifa kwa kufanya biashara na nchi za jirani, kwani Tanzania inapakana na nchi nane kati ya nchi hizo nne zinapakana na Tanzania kupitia Nyanda za Juu Kusini, nchi hizo ni Malawi, Msumbiji, Zambia na Kongo (Kongo Mashariki).  Lakini kati ya nchi hizo nchi mbili zinapakana na Mkoa wa Mbeya, na kabla ya mkoa huo haujagawanywa mwaka 2015 na kupatikana mkoa wa Songwe, Mbeya ilikua inapakana nan chi tatu ambazo ni Malawi, Msumbiji na Zambia.

Biashara za kimataifa kati ya nchi na nchi hufanywa kwa urahisi kwa nchi husika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi wa bidhaa, miundombinu hiyo ni kama vile; Bandari, Barabara, reli, na viwanja vya ndege. Licha ya Serikali ya Tanzania kuendelea kumairisha miundombinu hiyo kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini kama vileujenzi wa barabara za kimataifa (Tanzania-Zambia na Tanzania-Malawi), uimarishaji wa reli ya TAZARA inayoiunganisha Tanzania na nchi ya Zambia, ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Songwe.

Licha ya Serikali Kuchukua jitihada hizo za kimaendelo lakini bado kumekuwa na changamoto ya kusafirisha mizigo kutoka Tanzania kwenda katika nchi wateja kupitia upande wa nyanda za Juu Kusini, nchi hizo ni; Kongo (Kongo Mashariki), Malawi, Zambia Zimbabwe na Botswana kutokana na umbali uliopo toka bandari kuu ya Dar es Salaam. Hivyo ujenzi wa Bandari Kavu katika mikoa ya nyanda za Juu Kusini haswa Mkoa wa Mbeya ambako ndiko kwenye milango ya kuingilia na kutokea kwa nchi wateja zilizobainishwa hapo juu, ndio suruhisho pekee la kunusuru kuendelea kwa biashara kati ya Tanzania na nchi hizo kwani itasaidia kupunguzia kilomita 805 toka Dar es Salaam hadi Mbeya.

Juae Kheri MseseMeneja wa bandari kanda ya Ziwa nyasa, katika mkutano na wananchi wa kata ya Inyala tarehe 11 Agosti, 2017 amesema kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inakabiliwa na chanamoto kadha wa kadha lakini kubwa ni umbali uliopo toka Bandari ya Dar es Salaam kwenda katika nchi wateja hali inayoweza kusababisha wateja wengi kutotumia bandari ya Dar es Salaam na kuchagua bandari za nchi nyingine kutokana na gharama za kusafirisha mizigo.

"Changamoto tunazozipata katika masoko yetu katika nchi ya Malawi, Zambia, Kongo, na Botswana na Zimbabwe, sehemu zote hizo changamoto kubwa iliyokuwepo ni mfano katika nchi ya Malawi ni umbali kutoka katika bandari ya Dar es salaam kufika miji kama Lilongwe, na Blantaya. Mathalani kutoka Dar es Salaam mpaka Blantaya kuna takribni Kilomita 2000 na ukilinganisha na bandari za Nakala na Beira kuna kilomita 700 kwa hiyo unaona kwamba wananchi wa Malawi wanaweza kuchagua badari za Nakala na Beira kufanya biashara kuliko bandari yetu kubwa ya Dar es salaam. Sasa kwa kutambua hilo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kimkakati kabisa tumechagua ili eneo la Mbeya kuweza kuweka bandari kavu ambayo itakua inauwezo wa kuleta huduma karibu kabisa na tutapunguza takribani kilomita 1000 mtu kusafiri kwenda bandari ya Dar es salaam. Kwa maana hiyo tutaweza kuwahudumia vizuri wananchi wa Malawi, kwa maana Blantaya, Lilongwe na miji mingiine, lakini vilevile tutakuwa tumawasogezea karibu watu wa Kongo ambao tunapata changamoto katika upande wa Lobito na Welbis bay, lakini watu wa Zambia pia tutawasogezea hiyo mizigo kwa ukaribu zaidi"

**2.1 Eneo la mradi**

Mradi wa bandari kavu unatajiwa kujengwa katika Mkoa wa mbeya, Wilaya ya Mbeya kata ya Inyala, kijiji cha Makwenje. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 110 ambapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (PTA) imeridhia.

Eneo hili limetengwa baada ya kufanyika tathimini kwa kutumia picha ya anga, Tathimini iliyobainisha kuwa eneo hilo linafaa kwa Shughuli za bandari na kujengwa bandari kavu kwa sababu eneo hilo lipo karibu na barabara kuu ya Tanzania-Zambia, Tanzania-Malawi. Pia eneo hili limepitiwa na reli ya TANZARA, hivyo kushinda vigezo vyote vya kuwa Bandari Kavu.

**2.2 Faida za kuwepo Bandari Kavu Inyala**

- Kupunguza gharama kwa wateja za kusafirisha mizigo toka bandari ya Dar es Salaam kwenda kwenye maeneo yao
- Kuwabakisha wateja kuendelea kutumia bandari ya Tanzania kuliko kukimbilia katika bandari washindani za nchi zilizopo kusini mwa Afrika.
- Kuiongezea ufanisi bandari ya Dar es Salaam kwa kuipunguzia msongamano wa mizigo
- Kuiongezea kazi reli ya TAZARA katika kusafirisha mizigo toka Dar es Salaam kuileta kwenye Bandari kavu Inyala, Mbeya.

## 3.0 HATUA ZILIZOPANGWA KUFANYIKA ILI KUKAMILISHA UJENZI WA BANDARI KAVU INYALA

Katika ujenzi wa bandari kavu Inyala hatua kuu tatu zimepangwa kufanyika ili bandari hiyo iweze kukamili na kufanya kazi. Hatua hizo ni; Kutwaa eneo linalotarajiwa kujengwa bandari kavu, kulipa fidia na kuanza ujenzi wa miundombinu ya bandari kati eneo husika. Katika hatua hizi hatua ya kwanza itafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na hatua ya pili na tatu itafanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ambao ndio wasimamizi na waendeshaji wa mradi huo.

### 3.1 kutwaa eneo linalotarajiwa kujenga bandari kavu

Eneo lilipangwa kujengwa bandari kavu lenye ukubwa wa ekari 110 lililopo kijiji cha Makwenje kata ya Inyala linamilikiwa kimila na wanachi. Kwa mujibu wa Sheria ya Kutwaa Ardhi ya Mwaka 1967, inaeleza kuwa Serikali ikitaka kutwaa ardhi inayomilikiwa na wananchi haina budi kulitwaa eneo hilo kwa kulipa fidia kulingana na bei elekezi kama ilivyobainishwa kwenye kifungu cha 3 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, na pia kwa kuzingatia muongozo wa fidia wa mwaka 2012.

Kama ilivyoelezwa hapo juu kuwa hatua ya kutwaa eneo itatekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, hivyo Halmashauri hiyo haina budi kufanya mambo yafuatayo kwa ajili ya kulitwaa eneo hilo;

- Kufanya uhamasishaji kwa wananchi wamiliki na wanaolizunguka eneo hilo ili kuutambua mradi unaotarajiwa kujengwa
- Kuwatambua/kumtambua wamiliki/wamiliki wa eneo linalotarajiwa kujengwa mradi wa Bandari Kavu
- Kufanya tathimini kwa kila kipande cha ardhi kilichoendelezwa na kischoendelezwa kwa ajili ya kulipa fidia
- Kuandaa ripoti ya ulipaji fidia

### 3.2 Kulipa Fidia

Hatua hii inafanyika baada ya kukamilika kwa hatua ya kwanza, ambapo hapa wananchi wote waliotambuliwa kuwa ni wamiliki wa eneo hilo na kufanyiwa tathimini watalipwa fidia ya maeneo yao (fidia ya ardhi iliyoendelezwa na ardhi isiyoendelezwa) pamoja na posho mbalimbali kama zilivyoelezwa kwenye Sheria ya kutwaa maeneo ya Mwaka 1967. lakini si kila mtu anakuwa na sifa ya kulipwa posho bali inalipwa kwa watu wenye sifa maalumu kama inavyoelezwa hapo chini.

**Posho ya usumbufu,** posho hii inalipwa kwa kila mwananchi ambaye ambaye eneo lake linatwaaliwa na Serikali. Posho hii inalipwa kutokana na faida inayopatika kwa kuweka pesa kwenya akaunti ya amana ambayo inakuwa ni asilimia nane (8%) ya pesa inayofidiwa kwa mhanga.

**Posho ya upotevu wa makazi,** posho hii inalipwa kwa mhanga ambaye ameanzisha makazi katika eneo ambalo analipwa fidia (amefanya maendelezo ya kujega nyumba ana anaishi katika nyumba hiyo). Posho hii inalipwa ili kumuwezesha mhanga kupata sehemu nyingine ya kuishi wakati anafanya utaratibu wa kujenga nyumba nyingine. Hivyo atalipwa kodi ya pango ya miezi 36 (miaka mitatu).

**Posho ya upotevu wa faida**, posho hii inalipwa kwa mhanga ambaye amelifanyia maendelezo eneo lake kwa kuweka kitega uchumi kama vile mgahawa, nyumba ya kulala wageni, grosali n.k. Hapa mhanga atalipwa upotuvu wa faida wa miezi 36 (miaka mitatu). Posho hii inalipwa baada ya mtaalamu kufanya tathimini na kubaini faida halisi aliyokuwa anaipa mhanga katika biashara yake.

**Posho ya usafiri,** posho hii inalipwa kwa mhanga ambaye ameanzisha makazi katika eneo analolipwa fidia (amejenga na anaishi katika eneo hilo). Kwa lungha nyingine posho hii inaitwa posho ya usafiri ambayo inalipwa ili kumuwezesha mhanga kuhama katika eneo hilo. Analipwa nauli ya kusafirisha mizigo tani 12 katika kilomita 20.

**3.3 Kuanza kwa ujenzi wa miundombinu**

Hatua hii itatekelezwa baada ya kufanyika kwa hatua ya kwanza na ya pili. Hapa mradi uliokusudiwa unaanza kutekelezwa kwa hatua za ujenzi ambao utafanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa bandari Tanzania (TPA)

**4.0 KAZI ZILIZOFANYIKA**

Kulingana na hatua zilizopangwa kuchukuliwa ili kukamilisha mradi huu, kazi inayoendelea sasa ni kazi ya kulitwaa eneo kusudiwa. Katika hatua hii mambo kadhaa yameshakamilika, ambayo ni;

**Kufanya uhamasishaji,** kazi ya uhamasishaji imefanywa kwa kutekeleza kazi kuu nne ambazo zinajumuisha kikao kimoja na mikutano mitatu.

Kazi ya kwanza ilikua ni mkutano wa hadhara ulifanyika tarehe 11 Agosti, 2017. Mkutano huo uliwahusisha wananchi wote wa kata ya Inyala ambapo Mkuu wa Mkoa, Mhe. Amosi Makalla ndiye aliyekuwa muwasilisha mada mkuu. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kujenga bandari kavu Inyala.

Kazi ya pili ya uhamasishaji imefanyika kwa kufanya kikao na viongozi wa kijiji cha Makwenje ambapo ndipo eneo la mradi lilipo. Kikao hicho kimefanyika tarehe 18 Agosti, 2017 ambapo Mwenyekiti wa kijiji, Mtendai wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya kijiji, pamoja na wazee maarufu wa kijiji walihudhuria kikao hicho. Lengo la kikao lilikuwa ni kuwaeleza majukumu yao katika kukamilisha mradi wa ujenzi wa bandari kavu.

Kazi ya tatu ilikuwa ni kufanya mkutano wa hadhara na wananchi wa kijiji cha Makwenje. Mkutano huu ulifanyika tarehe 18 Agosti, 2017, lengo la mkutano huu lilikuwa ni sawa na lengo la mkutano uliofanyika tarehe 11 Agosti, 2017 lakini mkutano uliwahusisha wananchi wa kijiji cha Makwenje pekee.

Kazi ya nne ilikuwa ni kufanya mkutano na wananchi wanaomiliki vipande vya ardhi katika eneo kusudio la kujenga Bandari Kavu. Mkutano huu ilifanyika tarehe 11 Septemba, 2017. Lengo la mkutano huu lilikuwa ni kuwaeleza stahiki zao watakazozipata kabla ya eneo hilo kutwaaliwa na Serikali.

**Kazi nyingine iliyofanyika ni Kulibaini eneo na wamiliki wa eneo husika,** kazi hii imefanywa na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa kushirikiana na viongozi wa kijiji cha Makwenje. Kazi

imefanyika tarehe 30 Agosti, 2017 kwa kuweka alama kwenye eneo la mradi, kisha uongozi wa kijiji ukawatafuta wamiliki wa maeneo hayo.

**5.0 KAZI INAYOENDELA SASA**

Kazi inayoendelea sasa katika eneo la mradi ni kufanya uthamini, ambapo wataalamu toka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wapo katika eneo la mradi wakiendelea na kazi ya kumfanyia tathimini kila mhanga katika eneo lake. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Oktoba.

**HITIMISHO**

Bandari kavu tarajiwa ya Inyala itakuwa ni tawi la bandari kuu ya Dar es Salaam, ambapo inakadiliwa kuwa zaidi ya asilimia sabini ya mizigo inayopokelewa katika bandari kuu ya Dar es Salaam itasafirishwa kuletwa katika bandari kavu ya Inyala. Hivyo kuwafanya wateja wanaotoka katika nchi za Malawi, Zambia, Kongo Mashariki, Zimbabwe na Botswana kutofika Dar es Salaam, jambo litakalosaidia kumpunguzia mteja gharama za kusafirisha mizigo yake.

Hivyo shabaha ya Serikali ni kuukamilisha mradi huu kwa haraka ili biashara iendelee kushamiri, tunawaomba wananchi waiunge mkono Serikali yao kwani kufanikiwa kwa malengo ya Serikali ndiko kufanikiwa kwa maendeleo ya wananchi.